# *Ishara Kuu*

Asanteni sana. Na Bwana ambariki kila mmoja wenu.

Tunapoendelea kusimama kwa muda kidogo tu, hebu na tuzungumze na Mkuu huyu tunayemwabudu *sana* alasiri ya leo, Bwana wetu Yesu.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunainamisha mioyo yetu Kwako, na vichwa vyetu, ili tuweze kukuelezea Wewe, katika njia hii rahisi ya kuwasiliana kwa njia ya maombi, kwamba tunashukuru kwa yote ambayo masikio yetu yamesikia, na macho yetu yameuona Uwepo Wako pamoja na Kanisa Lako, katika siku hii ya mwisho, juu ya ishara hizi kuu za kuja Kwake. Na jalia uwe ni wakati wa furaha kwa Kanisa Lako, kwa maana imesemwa wakati mambo haya yatakapoanza kutimia, basi tuinue vichwa vyetu, ukombozi umekaribia. Nasi tunaomba ya kwamba huo ndio utakaokuwa msimamo wetu.

3 Nasi tunashukuru kwa yale uliyotufanyia, na yale matokeo ya Uwepo Wako yaliyoacha juu ya watu, na jalia sikuzote daima yawepo. Jalia wakupende daima, Yesu, kwa moyo wao wote. Siku moja, mimi, mtumishi Wako, itanibidi kuondoka, lakini kama utanichukua kabla sijapata nafasi ya kurudi tena, jalia wajue ya kwamba Wewe ni Mungu asiyepatikana na mauti ambaye hawezi kufa Nawe utakuwa pamoja nao milele. Na kama ikikupendeza Wewe, katika wakati mwingine, mtumishi Wako apate kurudi kuhudumu pamoja na watumishi Wako, ninaomba ya kwamba utatujalia hayo.

4 Mbariki kila mhudumu. Mungu, tunaomba ya kwamba kila mtu wa Mungu atatiwa mafuta upya kwa Roho Mtakatifu. Na kwamba, kama vile ndugu yetu ameelezea, kwamba vijana wanaume watasimama na kutiwa mafuta kwa Roho, roho ya Upendo, roho ya ushirika, roho ya nguvu, wapate kusaidia kuipeleka Injili hii ulimwenguni kote, kwa kuwa Bwana tunatambua ya kwamba leo huduma inahitajika, imechelewa kuliko tunavyodhania.

5 Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utayabariki makanisa yao hapa, na jalia kuwe na uamsho wa mtindo wa kale utakaotokea hapa Chicago, na jalia Roho Mtakatifu ashuke na kusababisha jambo hili kutukia. Ninaliombea tawi la Wafanyabiashara Wakristo, kwamba Wewe utawabariki, na jalia wawe vyombo vya kuwaingiza watu wengi katika ushirika wa Kristo, tujalie, Bwana, hao wote.

6 Asante kwa ajili ya ukumbi huu, na kwa wale walioturuhusu kuupata. Tunashukuru, Bwana, kuwa katika nchi huru bado, ambamo bado tunaweza kumwabudu Mungu kulingana na mwongozo wa dhamiri yetu wenyewe. Tunashukuru kwa ajili

ya wanaume ambao wangali wanaamini Ujumbe, na wanawake, wavulana kwa wasichana. Wabariki wahandisi hawa, mlinzi wa hili jengo, Baba, tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja nao, na kila mtu katika Uwepo wa Kiungu.

7 Asante Baba, kwa ajili ya karama za watu Wako ambao—ambao wamesaidia kuuendeleza mkutano huu, kila mmoja, Bwana, ninaomba ya kwamba utawabariki. Ninakushukuru kwa ajili ya sadaka ya upendo ambayo watoto Wako walinipa kwa maelekezo Yako. Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba itawarudia mara mia, na Utukufuni, ambako hazina zetu, hazina za kweli, zimewekwa, jalia wapokee baraka tele kutoka kwake.

8 Tusaidie sasa, na kulitakasa Neno ninapojikabidhi Kwake, na kwa Roho, ili tuweze kutoka hapa alasiri ya leo, kama wale waliotoka Emau, tukisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

9 Mnaweza kuketi. Asanteni sana kwa kuhudhuria kwenu kwema, kwa yote ambayo mmefanya na kusema, na kwa yote mliyotoa na kwa ushirikiano wenu. Ninataka kushukuru kundi hili zuri la ndugu, hapa nyuma, alasiri ya leo, kwa ajili ya uwakilishi huu mkuu wa huduma, ndugu wa imani moja ya thamani, wanaoitetea Injili ile ile tunayohubiri.

10 Mungu na azistahishe huduma zenu, popote mlipo, na awape watoto wachanga waliozaliwa upya kila wakati mnapohubiri. Ishara kuu za Pentekoste na ziinuke kanisani mwenu na mambo makuu ya ajabu yafanywe na Kristo. Jalia tawi hili lisife kamwe, tunajua Kanisa halitakufa, nami naomba ya kwamba hili tawi halitakufa, litashirikiana na Kanisa mpaka wakati utakapokuja. Mungu awe pamoja nao.

11 Na kwenu nyote watu wapendwa, mlinitumia zawadi ndogondogo: Ndugu fulani alinitumia lundo kubwa la biskuti, na, loo, vitu vingi sana, na zawadi ambazo watu wamempa Billy na hao wengine juma hili, kuingia katika matoleo ya Mungu, na kadhalika, na matoleo ya upendo, mnakumbuka jinsi yalivyo, ni matoleo yanayoenda kwa misheni za kigeni. Na halafu yale nisiyoweza kutumia tu kwa yale yanayonibidi kuwa nayo kwa ajili yangu na watoto, hayo mengine yanaenda kwenye umishenari wa nchi za kigeni kusaidia kuipeleka Injili mara tu ninapokuwa huru; nami ninajua hiyo ni mara moja, mnaona, ninajua tu jambo hilo.

12 Na kwa wale ambao hata hawawezi kununua chakula katika nchi za kigeni, kamwe hatuwaombi hata senti moja, tunaingia tu, tunadhamini kila kitu kwa pesa mlizonipa, kwa sababu ninajua itanibidi kuwajibika kwa ajili yake. Nami ninataka kuhakikisha ya kwamba yanatumika vizuri, maana mimi ndiye ninayepaswa kuwajibika, kama msimamizi wa fedha za Mungu.

Nami ninatumaini ya kwamba Mwenyezi atawabariki sana, kwa wingi, na sasa, neema Yake na ikae juu yenu.

13 Basi kumbukeni, wakati wowote ambapo mngetaka kunitumia kadi ndogo, ninii tu: Jeffersonville, Indiana, ukitaka, Sanduku la Posta 325. Hatujaribu, kupata anwani yako, kwa sababu nafikiri katibu wangu yupo hapa leo, wa kanisa, na, Ndugu Jim Maguire, nami najua tuna wakati mgumu kupata usaidizi wa kujibu hizo barua. Lakini tunapendezwa tu kujaribu kuwasaidia *ninyi*, kwa vitambaa vidogo tunavyoweza kuwatumia, ama swali.

14 Sasa, kama kuna swali lolote la Mafundisho, usiniulize, afadhali ungemwuliza mchungaji, unaona, kwa sababu ni—ni—ni, huo ni wajibu wake. Kama amewaleta salama umbali huu pamoja na Mungu, atawapeleka sehemu iliyosalia. Kwa hiyo ninyi, na kwa hiyo mnamwuliza tu mchungaji wenu Mafundisho, kwa sababu sipendi kujibu maswali hayo, kwa sababu huenda kukawa na kila mmoja wetu hapa juu, huenda tusikubaliane. Hakuna, hakuna vidole gumba vyetu viwili vinavyofanana, wanasema, hakuna pua zetu mbili. Nadhani mnafurahia jambo hilo, ndugu, hamna pua kama yangu.

15 Na kwa hiyo kuna . . . Huenda tusikubaliane juu ya kula, mtu anaweza kupenda sambusa ya tofaa, wakati hakika ninathamini hiyo sambusa kubwa, kali ya cheri niliyotumiwa muda mfupi uliopita. Ngojeni tu mpaka nitakapoanza kushuka barabarani! Na kwa hiyo ninaipenda kweli, nitakuwa na yubile ya ulaji bora kutokana na hiyo, Bwana akipenda.

16 Kwa hiyo, nina njaa kwa vyovyote vile, na wakati wa mikutano sili yapata mara moja kwa siku, na wakati mwingine mara mbili, kiamshakinywa kidogo chepesi, halafu yapata katikati ya mchana kitu chepesi, kisha nangojea mpaka kesho yake asubuhi, tena wakati mwingine hakuna kabisa. Mkutano uliopita, nilikuwa, naamini ilikuwa, mikate hii myebamba ya vanila na—na namna fulani ya maziwa ya unga, katika mkutano wote, ili niweze kuwa katika hali *nzuri sana*. Wanafunzi wadogo walikuwa wameketi pale, nami nilitaka kuwa *sawa* kabisa, ili kwamba kama Roho Mtakatifu alinena . . . Naye alinena. Hiyo ni kweli. Na kula tu kile nisichoweza . . .

17 Basi kumbukeni, marafiki, nimekuwa hudumani mfululizo tangu Krismasi, sikuzote nikiendelea tu mpaka nimechoka sana, nimechoka sana alasiri ya leo. Na itachukua muda mrefu sana kabla sijapumzika. Nina siku chache zijazo, ninatoka kwenda sasa hivi kwa ni—ninii chache, mapumziko ya siku tatu ama nne. Lakini mtu yeyote anajua ya kwamba huwezi kupumzika katika siku tatu ama nne, inakubidi kuchukua mapumziko kamili na kujijenga tena.

18 Basi mnaona, mnaona tu papa *hapa*, yaliyo papa *hapa*, yanayotukia *hapa*. Mbona, siku nzima katika mahojiano hayo,

kuna mara nyingi, nyingi, nyingi zaidi. Na *hapa* unaona tu baadhi, Roho Mtakatifu anamwita mtu fulani, na kusema jambo fulani na kuwahusu namna hiyo, lakini katika mahojiano hayo ya faragha kuna watu ambao ni Wakristo, labda, na, lakini wa—wana kitu fulani maishani ambacho kwa kweli hawawezi, hawawezi kukiondoa, hawajui waende wapi, nao hawana budi kupata Neno kutoka kwa Mungu.

19 Nami laiti ningaliweza kusema, "Shuka uje," juu ya mmoja, lakini rafiki, kuna yapata, nafikiri katibu wangu huko nje anasema, kuna mia sita na kitu, wakingojea kutoka kote ulimwenguni. Basi mnaona? Na kwa hiyo ni . . . Lakini tutafurahia kuweka jina lako kwenye orodha, na kadiri tu tunavyoweza kuwafikia. Na mtu fulani . . .

20 Mwajua, Biblia inasema mambo fulani, lakini kama . . . Kuna mambo yaliyofungiwa maishani, kama vile zile amri, walikuwa na zile amri kumi, lakini basi Mungu alikuwa na mwonaji ambaye wakati kitu fulani kilipotokea ambacho hakikuandikwa kwenye zile amri, basi Neno la Mungu lilikuwa pamoja na nabii aliyelifunua, jinsi lilivyopaswa kuwa.

21 Wala Mungu habadiliki, angali ana njia zile zile, ziko, kama tukizifungua tu, hivyo tu. Hilo ndilo tunalohitaji leo hii ni kufunguliwa kwa njia, kama nilivyosema hivi majuzi usiku kuhusu, "Endeleeni kuchimbua, kuchimbua mabonge yote." Bado tuna ninii . . . Njia ziko hapa, na zote zimefunguliwa pale Kalvari, na—na zilifunguliwa nyikani, nazo zitakuwa wazi leo kama tutaondolea tu vitu hivyo mbali, kutokuamini kwetu kwote, na kuamini ya kwamba Mungu angali ni Mungu.

22 Na kama ungetaka niombee kitambaa na kukutumia, nitafurahi kufanya hivyo. Ninaona kila usiku na mchana wana vitambaa vilivyowekwa hapa juu. Tunavituma kwa maelfu, kote ulimwenguni. Navyo vinaweza kufanya zaidi ya tuwezavyo sisi, jambo pekee ni kuwasiliana tu na watu, mambo mengi makuu hutokea. Ni bure, hakuna chochote tulicho nacho chetu wenyewe tunachouza.

23 Tuna vitabu kadhaa hapa, wanaviuza, bali si vyetu, ni vya Bw. Stadsklev, na Bw. Lindsay, na vingine mbalimbali, ambavyo tunavinunua kutoka kwao kwa punguzo la senti arobaini, asilimia arobaini, ndipo inatubidi kulipa *kiasi fulani* kwa juma kwa wavulana kuviuza, na *kiasi fulani* kwa kuvibeba, *kiasi fulani* kwa ajili ya kuvisafirisha, hata hupati faida kwake, hivyo tu, mkutano hauna budi kusaidia kushikilia hilo.

24 Halafu basi daima nimesema, ya kwamba kama kuna mtu yeyote anayekuja, kwa Leo, na Gene, na hao wanaouza hivyo vitabu, nao ni mawakala wa kulipwa, na kanisa, kuuza vitabu, kama mtu fulani akija, mama, baba, ama mtu fulani, nao waseme, "Ningetaka kupata kimoja, lakini sina hata senti moja, ninaninii tu . . ." wape kwa vyovyote vile, hebu

wakichukue. Hata hivyo, ni kwamba tunajaribu kulieneza Neno la Mungu, mahali fulani, sehemu fulani ya sadaka, ama kitu fulani kitavilipia. Ndipo zilizosalia, basi tunaziwekeza tena katika vitabu vingine ambavyo mtu mwingine huchapisha, nasi tunavinunua kutoka kwao, sivimiliki, vinatoka kwa mtu mwingine.

25 Kwa hiyo ninawathamini wote, na ninii wangu, bila shaka, wahudumu wenzangu, Ndugu David duPlessis, na Ndugu Boze, na wengi wa wahudumu mashuhuri hapa Chicago ambao nimekuwa na majaliwa ya kukutana nao. Baraka nyingi sana za Bwana ziwe juu yenu, watumishi Wake, na juu yenu, watu Wake.

26 Sasa, si—sina budi kuharakisha kidogo alasiri ya leo, kwa sababu hatutakuwa na wakati. Na mimi—mimi bila shaka ninawaheshimu ninyi watu mnaokuja hapa, na ko—ko—ko—kondoo wa hawa wachungaji hapa, ambao Mungu amewapa, kwa Roho Mtakatifu, usimamizi. Nasi tutajaribu kuwaachilia mapema vya kutosha ili mweze kwenda nyumbani na kwenda kanisani, usiku wa leo. Na hizo, nafikiri, zilikuwa kanuni za Wafanyabiashara Wakristo, tumekubali hilo muda mrefu uliopita, kama si za makanisa. Sasa, hata wakati makanisa yote yanaposhirikiana, tungali tunapendelea Jumapili alasiri, kwa hiyo watu. . .Nafikiri kila mtu anapaswa kuhudhuria kanisa lako, nafikiri hapo ndipo mahali pako, wajibu wako.

27 Sasa, alasiri ya leo ningetaka kusoma, ninayo mafungu yaliyoandikwa hapa, na Maandiko kadhaa, na marejeo madogo, na kadhalika, nami ningewatakeni, kama mnaandika mambo haya, na kama mtanipa usikivu wenu wote upesi tu kadiri Roho Mtakatifu atakavyoniruhusu kumaliza, mfungue pamoja nami katika Isaya, mlango wa 7 na kifungu cha 14, ningependa kusoma kwa—kwa ajili ya somo la Maandiko.

> *Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara; Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.*

28 Nami ninataka kuzungumza alasiri ya leo juu ya somo la *Ishara Kuu,* kama ningeweza kuliita somo, ama fungu: *Ishara Kuu.*

29 Hii ni siku ya—ya mambo *makuu.* Kila kitu hakina budi kuwa kikuu, ama kama hawana. . .kama si bidhaa kuu, hakitauzika. Nasi tunakumbuka, ya kwamba kwa sababu wanadamu, Mungu akijua tabia yao, na kitu fulani ndani ya mwanadamu ambacho haijalishi ameanguka umbali gani, hata hivyo katika maumbile, yeye ni mwana wa Mungu, kimaumbile, Mungu alimwumba katika mtindo Wake Mwenyewe.

30 Na wakati mwingine tunaangalia chini kwenye nyumba zetu nzuri. Mara nyingi ningeshuka kwenda Miami, Fort Lauderdale, huko Florida, na hao watu huko chini wanashughulikia vizuri zaidi kitalu chao cha nyuma kuliko, na kukata nyasi zao

kuliko nifanyavyo ninii zangu, nywele zangu zilizosalia, laini kama unyoya, huku watu wengine wakiokota tu kila jani dogo; majengo mazuri yenye—yenye picha kubwa mno ambazo huenda zikagharimu maelfu ya dola; mitende iliyozungukwa na mstari wa taa za neoni kuizunguka; na taa kubwa zenye mwanga mkali usiku kuakisi mng'aro wa upinde wa mvua, na taa nzuri; pamoja na jahazi kwenye kitalu cha nyuma, zikipitia kwenye mfereji, kutoka kwenye rasi kuu ya maji, zikiingia.

31 Nami nikasimama na kuwazia yapata miaka mia tatu iliyopita hapo palikuwa ni kinamasi, cha *kale*, mamba wa maji baridi, mamba wa maji ya chumvi, vinamasi. Watu wanaingia mle pamoja na mitambo na—na kuchimbua vichaka vyote vichafu, na kadhalika, na—na kuchukua blowa kubwa na kulipulia mbali mchanga huu, na kuweka misingi na kujenga makazi, na kujenga barabara zilizoinuka, na kadhalika, wanajenga majengo ya kupendeza. Ni kitu gani kinachofanya hivyo? Kwa sababu ndani yake, yeye ni muumba mdogo. Hawezi kuumba, bali anaweza kuchukua kitu ambacho tayari kimeumbwa na karibu afanye kiumbe kingine kutoka kwake, bongo lake, akili zake.

32 Sasa, tunaona tofauti: Mnyama kamwe habadilishi makao yake, mbweha angali anaishi kama alivyoishi maelfu ya miaka iliyopita, ndege angali anajenga kiota cha aina ile ile, nao samaki wangali wanatagia mchangani, nyani angali anaishi mtini, nasi tunaona uhai wa wanyama ni mambo ya kale tu, bali mwanadamu yuko katika mfano wa Mungu, kwa hiyo anaendelea kujenga.

33 Kwa hiyo siku hizi tumefikia mahali ambapo kila kitu tunachozungumzia ambacho kina thamani yoyote ya mauzo, ni *kikuu*. Tunaenda kwenye supamaketi, lile duka dogo la pembeni limeishiwa na biashara. Supamaketi haina budi kuwa kubwa mno, kitu *kikubwa*. Unanunua stempu, unazilipia kila moja nikeli, stempu za biashara. Usifikiri wanakupa kwa sababu hawakupi, unazilipia, gharama kubwa. Lakini macho ya umma ndiyo yanayopaswa kuyaona, televisheni, magazeti.

34 Hivi majuzi, nilikuwa nikisikiliza matangazo ya redio, walisema, "Usiwe wa mtindo wa kale, tumia sabuni mpya. Hakuna kuosha, hakuna kupangusa, vitumbukize tu majini, vyombo, ni safi kabisa na yote unayopaswa kufanya ni ninii tu, vema, vitumbukize tu majini, ukavianike kwenye rafu, viko sawa. Loo, usiwe wa mtindo wa kale."

35 Tangazo hilo la biashara lilitolewa kisha lingine likatokea, nalo likasema, "Usichome mikono yako mirembo kwa sabuni hizi mpya, tumia sabu-. . .aina nyingine ya ninii, Oksidoli ya mtindo wa kale." Kasema, "Kwa sababu, angalia vile mikono ya nyanya inavyoonekana, angalia jinsi mikono ya mama inavyoonekana, walitumia mapovu ya sabuni, usiichome,

mikono yako kwa sabuni hizi mpya walizo nazo." Na Colgate-Palmolive-Peet iliandika makala yote mawili, inayotengenezewa papo hapo Jeffersonville.

36 Mnaona, watu wanapenda kudanganywa. Naye ibilisi amewaweka katika hali hiyo ili kwamba wakati kitu *halisi* kinapokuja, wangali wanafikiri wamepumbazwa. "Wale wamngojeao Bwana!" Wale wamjuao Mungu watafanya mambo makuu.

37 Lakini tuko katika mambo *makuu*: mauzo makuu, makuu, makuu, makuu, makuu, makuu, kila kitu ni kikuu, magari makuu, jeti kuu, loo, jeti kuu, spidi kubwa mno, kila kitu ni *kikuu*. Jamii kuu, loo, kila mtu anataka kuwa jamii kuu. Hitler aliwaambia tu Wajerumani kwamba walikuwa ni watu wakuu sana, wakakuta kwamba hawakuwa. Vikuu, vikuu, kila kitu ni kikuu.

38 Na sasa, yote yanajumuika kwenye hisia, kama tu utasimama na kuchunguza. Kwa sababu ni baadhi ya viumbe ambavyo Mungu aliviumba, navyo viko katika wazo hilo la mambo *makuu*, halina budi kuwa *kuu*. Kwa hiyo mambo haya yote yanamaanisha jambo moja: ni ishara. Ni ishara ya giza kuu linalokuja, giza kuu. Wana . . .

39 Adamu alilianzisha katika bustani ya Edeni, alitaka dini kuu. Na kila kitu ni kikuu, kikuu. Basi inamaanisha tu kwamba tunaingia tu gizani pamoja na mambo haya makuu, maana wana bunduki kuu ambayo itafyatua seli kuu, ambayo italipua anga kuu, na, loo, kila kitu ni mfyatulio mkuu sana, kuua. Loo! Mwanadamu daima amejaribu kufanikisha jambo kuu sana mwenyewe, hataki kamwe kuchukua njia ya Mungu kulihusu, anataka kufanikisha jambo fulani yeye mwenyewe.

40 Adamu alikuwa na dini kuu mno, alikuwa na dini aliyojiundia mwenyewe, wakijaribu kuwa na dini kuu mno bila upatanisho kwa ajili ya dhambi. Mwanadamu ana jambo lile lile, akijaribu kufanya hivyo leo, kuwa na dini pasipo upatanisho. Huna budi kuwa na upatanisho, na wakati upatanisho unapokugusa, umetakaswa na dhambi na kutokuamini. Lakini Adamu alitaka kitu fulani kikuu, kitu fulani alichofanya mwenyewe, alitaka kufanikisha jambo fulani, hilo liko *ndani* ya mwanadamu. Adamu alionyesha hilo, wakati alipojitengenezea nguo za majani ya mtini za kuvaa. Tunaona ya kwamba alitaka jambo hilo kuu, jambo alilotaka kufanya mwenyewe.

41 Baadaye kidogo katika Mwanzo tunaona mtu jina lake Nimrodi, alitaka kujenga mnara mkubwa mno. Alitaka kujenga kitu ambacho angeweza kuuachia ulimwengu, "Mnaona kile *mimi* nilichofanikisha, kitu ambacho nimefanya *mimi*. Sasa, ninyi watu endeleeni na kuishi vyovyote mtakavyo, na kama Mungu akipata dhana ya kutuangamiza, tutakimbia tu moja

kwa moja tupande mnara huu, tutakuwa huru kabisa na mafuriko yote. Ishini mtakavyo."

42 Hivyo ndivyo mwanadamu anavyojaribu kufanya leo na dini yake kuu, "Ishi utakavyo, tunaye mtu mtakatifu anayewaombea, kasisi, askofu, ama mtu fulani. Endelea tu, tuna maagizo makuu, tuna makanisa makubwa sana na madhehebu makubwa. Endeleeni tu, maadamu wewe ni mfuasi wake, ni sawa." Mtaona ya kwamba yataanguka kama mafanikio ya kila mtu, hayana budi.

43 Ndipo baada ya hayo, akaja mtu jina lake Nebkadreza, ambaye alidhani angeweza kujenga mji mkuu mno, kitu fulani cha kufanikisha mwenyewe. Siku moja alitoka nje na kusema, "Mnaona kile *mimi* nimefanya?" Ndipo Mungu akaubadilisha moyo wake ukawa moyo wa mnyama.

44 Alikuwa na wanasayansi bora sana ambao ulimwengu ulikuwa nao, kama vile Nimrodi alivyofanya kuujenga ule mnara, naye Nebkadreza akawachukua wanasayansi walio bora sana, jeshi lililo bora sana, mitambo bora sana ambayo ingepatikana, akaiweka yote ndani ya ukuta mkubwa mno, hata walisema wangeweza kufanya mashindano ya magari ya farasi juu ya huo ukuta, naye akaweka kila kitu mle ndani. Walifanya nini mara walipoingia mle? "Ishini vyovyote mtakavyo. Hakuna taifa lingine linaloweza kutusumbua, hakuna yeyote aliye nje anayeweza kuingia. Tumeushinda ulimwengu." Ilikuwaje usiku mmoja? Kumbukeni, Mungu anaweza kuona kutoka huko juu.

45 Basi walipokuwa na kipindi cha televisheni, walitaka kufanya mizaha kuhusu dini, ndipo wakaenda wakachukua vyombo vitakatifu vya Mungu, wakaanza kuvifanyia mzaha, kwa kuvinywea divai, ndipo kukatokea maandishi ya lugha isiyojulikana ukutani, na jamii yao yote kuu haikujua maana yake. Lakini walikuwa na mtu mmoja miongoni mwao ambaye angeweza kufasiri lugha zisizojulikana, Danieli. Basi kumbukeni, hivyo ndivyo Kanisa la—la Mataifa lilivyoingia, na hivyo ndivyo linavyotoka.

46 Na katika hii karamu kuu ya Belteshaza, Mungu alishuka na kuwaagiza Wakaldayo na nanii . . . wachimbe mahali hapo, na kuyaondoa maji, wapitie chini ya lango. Mji huo mkuu haukuwa kitu, kwa hiyo siku hizi ni magofu.

47 Nchi yetu yenyewe tunayoipenda hapa, kwa kuwa tulitoka Uingereza, ambayo iliitwa "Malkia wa baharini" siku hizo, nayo ingali inajiita, "Malkia wa baharini," tulitaka kuwashinda kwa hiyo tujijengea meli kubwa mno. Tulifanikisha kitu fulani kujenga meli kubwa mno ambayo wanasayansi wetu, na wataalmu wetu mashuhuri walisema haingeweza kuzama. Mungu kwa mkono Wake wenye nguvu alionyesha ya kwamba haijalishi kile mwanadamu anachoweza kufanikisha kimeingia mavumbini, ile *Titaniki* ilizama kama mafanikio mengine yote

ya mwanadamu. Meli yetu kuu mno haikufaidi kitu, ilifanya safari moja, ama kitu kama hicho, kisha ikagonga siwa barafu ikazama chini ya bahari.

48 Ufaransa ilijaribu kujenga Ngome ya Siegfried, Ujerumani, Ngome ya Maginot. Baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, basi Ufaransa ingali ilitaka wanawake wao, divai, na anasa, ndipo wakaijenga hiyo Ngome, na kuelekeza bunduki zao zote Ujerumani, "Hima sasa, hebu tule, tunywe, na tufurahi, kila kitu ni sawa kabisa." Ilikuwaje? Ujerumani ilizunguka moja kwa moja nyuma yake, walisahau jinsi ya . . . kuacha mahali pa kugeuzia bunduki zao, ndipo Ujerumani ikaibomoa. Ujerumani baadaye ilijenga Ngome ya Maginot, kombora angamizi la Marekani likaibomoa kabisa.

49 Kwa hiyo mnaona, kila kitu ambacho mwanadamu anajaribu kujificha nyuma yake kwa mafanikio yake mwenyewe, ha—hana budi kushindwa. Laiti ningalikuwa na elimu ya kutosha kuweka hili jinsi ni—ni—ninavyolijua kuwa, natumaini yale ninayopungukiwa katika elimu, Roho Mtakatifu atayafunua, kwa Utu Wake, ili mweze kuona kitu chochote cha kujibunia hakina budi kuporomoka. Naye mwanadamu daima, kwa asili yake, anajaribu kufanikisha kitu anachoweza kuacha kwa ajili ya kumbukumbu ya jambo fulani alilofanya.

50 Kanisa limejaribu kufanikisha jambo fulani. Wamejaribu kufanikisha dhehebu kwa nadharia za kujibunia, kwa elimu, kwa theolojia ya kujibunia. Kufanikisha! Kila mtu akifanyia kazi shirika lao. Limekuwaje? Katika jambo hilo lote, Mungu yuko wapi? Kila kanisa, na kila kanisa linataka mchungaji wao awe Ph.D., LL.D., ambalo ni sawa mradi tu una hizo pamoja na Mungu. Lakini unapoingia katika tamaa hizi za kujaribu kujenga kitu fulani wewe mwenyewe, kuonyesha ya kwamba madhehebu yako ni werevu zaidi, umati uliovalia nadhifu zaidi, maadili ya juu zaidi, meya wa jiji huhudhuria kanisa lenu, uko kwenye mchanga unaodidimia. Msisahau hilo, Chicago, kama sitazungumza nanyi tena, kumbukeni hilo! Vitu hivyo havina budi kuzama na kutoweka.

51 Wabaptisti wanafikiri watajijengea madhehebu, Wamethodisti vivyo hivyo, Wakatoliki vivyo hivyo, Wapresbiteri vivyo hivyo, Wanazarayo, Wapentekoste, Pilgrim Holiness, yote hayo, mafanikio fulani ya kujibunia. Lakini bila shaka litaporomoka tu kama ule mnara wa Nimrodi ulivyoporomoka, na mji wa Nebkadreza ulivyoangamia. Kama vile *Titaniki* ya Marekani ilivyozama, ndivyo watakavyozama, hayana budi kuzama, kila mafanikio ya kujibunia.

52 *Titaniki* iko wapi leo? Chini ya bahari. Uko wapi mnara wa Nimrodi? Umeanguka ardhini. Uko wapi mji usiopatikana na mauti wa Nebkadreza? Ulizama. Iko wapi Ngome ya Siegfried ya Ufaransa? Imelipuliwa vipande-vipande. Iko wapi Ngome

ya Maginot ya Ujerumani? Imelipuliwa vipande-vipande. Liko wapi kanisa la kimadhehebu? Limekufa. Ni kitu gani? Yote ni kumbukumbu ya kihistoria. Yote yaliyosalia kwenye Ngome ya Siegfried ni historia. Yote yaliyosalia kwenye Ngome ya Maginot ni historia. Yote yaliyosalia kwenye hiyo minara ni historia.

53 Na yote kanisa liliyo nayo siku hizi ni historia, yale Moody aliyosema, yale Sankey aliyosema, yale Finney aliyosema, yale Smith aliyosema, yale *Fulani-wa-fulani* aliyosema, ni historia. Lakini Mungu angali anaishi vivyo hivyo Naye daima ataishi. Ni historia: "Tulianza mwaka wa 1909." "Tulianza, huko nyuma kabisa katika wakati wa Luther." "Tuliaanzia kwenye. . . " Loo, jamani! Mungu kamwe hakuanza wala hatakuwa na mwisho. Kila kilicho na mwanzo kina mwisho, bali ni yale mambo ambayo hayakuanza kamwe ndiyo hayana mwisho.

54 Hiyo ndiyo sababu haidhuru tunapata mafanikio kiasi gani katika ulimwengu huu katika kujenga mazao yetu, madhehebu yetu, majengo yetu, miundo yetu, yote huanza na yote huisha. Nasi tulikuwa na mwanzo na mwisho, lakini tunapompokea Kristo tunampokea Mungu, Mungu ni wa Milele, nasi tunakuwa wa Milele pamoja na Mungu kupitia Uzima wa Milele, ambao kamwe haukuanza wala hautaisha kamwe.

55 Msiache hilo liwaondokee, liwekeni akilini mwenu na mioyoni mwenu likiwa safi, mradi tu mnaishi: Kila mafanikio ya kujibunia hayana budi kuanguka. Lakini liko ndani yake kufanya hivyo, kufanya hilo, Adamu, baba yake, alithibitisha jambo hilo. Yeye asingeendelea tu na kufanya mapenzi ya Mungu, kufanya yale Mungu aliyosema, naye alipoona alikuwa amekosea, basi alijaribu kufanya njia yake mwenyewe, akajaribu kuacha kumbukumbu, "Mimi ndimi niliyeanzisha dini ya Adamu." Loo, ingali hapa, bila shaka iko. Ingali hapa, tungali tunayo, nadharia za kujibunia pasipo na upatanisho.

56 Loo, wanadai upatanisho. Lakini upatanisho husafisha na dhambi, na dhambi ni kutokuamini, na wakati mtu anapokuwa asiyeamini Neno la Mungu, akisema ya kwamba Yesu Kristo si yule yule, katika nguvu zile zile, yeye ni asiyeamini. Huenda akawa mfuasi wa dhehebu lililo kubwa kuliko yote na awe na Ph., L.L.D, huenda akawa ni profesa, askofu, ama chochote kile, yeye angali ni mwenye dhambi asiyeamini.

57 Yesu aliuambia mfumo huo wa kujibunia katika siku Zake, walikuwa watakatifu, usingeweza kuwagusa, watu wenye uchaji, watakatifu, na wasio na lawama, Yeye akasema, "Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi," kwa sababu hawakumwamini. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililofanyika mwili, akiishi hapa duniani, miongoni mwetu, Neno la Mungu.

58 Loo, yote yamekuwa historia sasa; Mungu anabaki. Lakini katika hayo yote, kama vile umeme uliogawanyika katika usiku wenye dhoruba unavyomulika, inaonyesha kunaweza kuwa na

nuru gizani, inathibitisha ya kwamba hata iwe giza jinsi gani, bado kunaweza kuwa na nuru.

59 Kwa hiyo watu wakitaka kufanya ishara na kuwa na ishara, Mungu alisema, siku moja, "Nitawapa ishara kuu mno ya Milele. Nitawapa ishara, nayo itakuwa ni ishara kuu mno, ishara ya milele. Kamwe haitabadilika, itabaki vile vile jana, leo, na hata milele. Nitawapa ishara." Hawataipokea, bali hata hivyo Mungu anawapa.

60 Haidhuru hawakuipokea kiasi gani, ilikuwa pale vivyo hivyo tu. Haidhuru hawaipokei jinsi gani leo, nao wanataka mafanikio ya kujibunia, ishara ya Mungu ingali inabaki vile vile, ishara kuu, si kitu kilichopigwa msasa cha ulimwengu pamoja na elimu nyingi, na mafanikio ya kujibunia, si hayo, si mambo ya ulimwengu, wala chochote kilichobandikwa kwa ulimwengu. Yeye alisema, "Mimi si wa ulimwengu huu."

61 Vema, itakuwa ni kitu gani? Itakuwa ni Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu. Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu, hiyo itakuwa ndiyo ishara kuu mno: Mungu katika mwili. Inapaswa kuwa ya kushangaza kwa ulimwengu, Yehova, Mungu akifanyika Mmoja wetu, akabadilisha kinyago Chake kutoka kwa Yehova mkuu, asiyepatikana na mauti akawa maskini mtoto mchanga. Angeweza kuja na gwaride zima la Mbinguni kama angetaka. Kila Malaika, kila Malaika Mkuu wa Mbinguni angesimama miguu sawa, nazo baragumu zingebidi zitoe sauti ambayo ingeitikisa dunia, kama Yeye angalichagua kuja namna hiyo.

62 Angeweza kuja kwa mng'ao na fahari, bali hakuja hivyo, alileta ishara kuu. Angeweza kuja huku baragumu zikipigwa, dunia ikitikisika, akishuka kwenye ushoroba wa dhahabu kutoka Mbinguni na ulinzi wa Malaika, Makerubi warukao wamefunika uso wao kwa mabawa na juu ya miguu yao, wakipiga makelele juu Yake, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Wewe, Bwana Mungu, aliyekuwako, ambaye yupo!" Angeweza kuja namna hiyo kama angalitaka.

63 Mungu angeweza kuja hivyo, lakini Yeye alisema, "Nitawapa ishara kuu, nitawaonyesha ya kwamba vitu vyao vya kujibunia ni vya kipumbavu, mapambo yao yaliyong'arishwa, hayafai kitu. Nitawapa ishara kuu." Loo, angeweza kuja kama Malaika, bila shaka, angalikuja kama Malaika mkuu, anayeangaza, akielea hewani. Kila mtu angaliamini hilo basi, lakini Yeye alitoa ishara kuu ili yapata moja juu ya kumi waweze kuiamini. Mnaona, kile mwanadamu anachokiita kikuu, Mungu anakiita kipumbavu, na kile mwanadamu anachokiita kipumbavu, Mungu anakiita kikuu.

64 Sasa, hatuwezi kulikanusha neno la Isaya hapa, wakati Mungu aliposema kupitia Isaya, "Nitawapa ishara ya milele," ya milele, "bikira atachukua mimba, naye atazaa Mwana, naye

ataita Jina Lake Imanueli. Nitakuwa ndani Yake." Mungu pamoja nasi, ishara kuu, si msomi hodari, bali ishara kuu.

65 Hakuna kumbukumbu ya Yeye kwenda kwenye seminari yoyote, hakuna kumbukumbu Yake ya kupata kujifunza theolojia yoyote ya kujibunia, lakini kwenye umri wa miaka kumi na miwili, Yeye alikuwa amesimama pamoja na wenye hekima, akibishana nao, nao wasingeweza kulistahimili Neno Lake. Amina. Hiyo hapo ishara yenu kuu: kudumu na Neno.

66 Wanasema, "Siku za miujiza zimepita," na mambo haya yote, hebu na wayathibitishe. Um-hum. "Nitawapa ishara ya milele, ile ishara kuu." Loo, naam. Sasa, Yeye angeweza kuja kama Malaika, Angeweza kuja vyovyote alivyotaka, bali alichagua kuja kama Uzao wa Ibrahimu, amina, Uzao mkuu wa Ibrahimu. Hiyo ni kweli. Jinsi alivyochagua kuja kuonyesha katika siku hizi za mwisho ishara kuu za Mungu, jamii kuu, loo, naam, si kile mnachokiita jamii kuu, bali kile Mungu anachokiita jamii kuu. Kwa sababu walipata nini? Nguvu za kimbinguni, pamoja na ishara za kimbinguni, kupitia imani ya kimbinguni katika Neno la kimbinguni, kutoka kwa Mungu wa kimbinguni. Amina. Nena kuhusu *mambo makuu*! Whiu!

67 Mungu wa kimbinguni, katika mwili wa kimbinguni, ndani ya watu wa kawaida, akitoa ishara za kimbinguni. Haleluya! Naam. Jamii kuu, wale wamjuao Mungu wao watafanya mambo makuu, mambo makuu, kuonyesha ishara za kimbinguni, watu, Uzao wa Ibrahimu, ishara ya Kristo wa kimbinguni aliyefufuka katika wafu kimbinguni.

68 Na baada ya miaka elfu mbili, wale wakosoaji waliojaribu kumwua kule chini wanajaribu kufanya jambo lile lile siku hizi, bali ishara zile zile, ishara ile ile ya kimbinguni ingali inaonyesha miongoni mwa watu wa kimbinguni, ambao ni Uzao wa Ibrahimu. Amina. Najisikia vizuri. Amina. Mambo ya kimbinguni, ya kimbinguni, usipoamini mambo ya kimbinguni, unawezaje kumwamini Mungu? Kuzaliwa kimbinguni, kwa kuzaliwa kimbinguni, kwa nguvu za kimbinguni. Nena kuhusu mambo *makuu*!

69 Ni kitu gani kilicho ndani ya mwanadamu? Anataka mambo makuu, kwa hiyo anafanya nini na mambo yake makuu? Anaelekea mautini nayo. Ati nini? Mungu alijua hilo hapo mwanzo, kuwapa watu Wake aliye *Mkuu*, *Mkuu* aliye mnyenyekevu na mpole apate kuwapeleka Uzimani, sio mautini. Loo! Amina. Wa kimbinguni!

70 Sasa kumbukeni, kulikuwako na uzao wa kawaida wa Ibrahimu na Uzao wa kimbinguni wa Ibrahimu. Sasa, uzao wa kawaida wa Ibrahimu, kulingana na Mwanzo 22:16 na 17, Yeye alisema, "Uzao wako utamiliki mlango wa adui wake." Wakati alipomtoa Isaka dhabihu katika Mwanzo 22:16, 17, Yeye alisema, "Uzao wako utamiliki mlango wa adui wake." Mnalipata? Sasa,

uzao wa kawaida wa Ibrahimu ulikuwa ni Isaka, kwa hiyo kupitia kwa uzao wa Isaka, tunaona ya kwamba kweli walimiliki malango ya adui wao.

71 Wakati mmoja walikuwa na watatu wa hao huko Babeli, katika mji huo mkubwa kule, uliojengwa mji mkuu sana, bali walikuwa na wa kimbinguni. Nao wakawatupa kwenye moto mkubwa ulioongezewa moto mara saba kuliko kawaida yake, ndipo kulikuwa na ishara ya kimbinguni ya Mungu wa kimbinguni akisimama katika huo moto, akiwaokoa kimbinguni. Amina. Walifanya nini? Walimiliki malango ya tanuru, adui wao.

72 Kulikuwako na mwingine aliyeshuka kule chini, jina lake Danieli, uzao wa Ibrahimu. Ilikuwaje kwake? Alidumu mwaminifu kwa Mungu, alijua ya kwamba alikuwa ni uzao wa Ibrahimu, alijua alikuwa akifanya mema. Wakamtupa katika tundu la simba, na Nuru ya kimbinguni, mnyama anaogopa nuru, mwajua, kwa hiyo Nuru ya kimbinguni, Malaika wa kimbinguni alishuka kwa mtu aliyeamini mambo ya kimbinguni, ndipo mambo ya kimbinguni yakamwokoa. Naye akakaa usiku kucha katika tundu la simba, naye akatolewa nje kimbinguni kesho yake asubuhi, kwa sababu aliamini na kumtumainia Mungu wa kimbinguni, naye akamiliki mlango wa tundu la simba. Naam.

73 Kulikuwa na mtu jina lake Musa aliyeamini katika Mungu wa kimbinguni, alikuwa amekutana Naye na kuzungumza Naye kwa njia ya kimbinguni, kwenye kichaka cha kimbinguni, kilichokuwa na Moto wa kimbinguni kichakani. Naye akapata ujumbe wa kimbinguni, wa mtu mmoja, akishuka kwenda, uvamizi wa mtu mmoja kuiteka Misri, ujumbe wa kimbinguni, bali ulitoka kwa Mungu wa kimbinguni.

74 Kwa hiyo akashuka akaenda kule na kufanya jambo la kimbinguni, kwa sababu alileta ishara za kimbinguni, haleluya, juu ya watu wa kawaida, nao wakawakomboa Israeli kimbinguni. Wakati kitu chochote cha kawaida kilipoingia njiani mwake, njia . . . Alikuja kwenye lango la Bahari ya Shamu, bali aliamini katika Mungu wa kimbinguni, naye akaendelea kuelekea baharini, nazo nguvu za kimbinguni za Mungu wa kimbinguni zikafanya tendo la kimbinguni na kumkomboa. Whiu! Utukufu! Hiyo ni kweli.

75 Jinsi gani? Kwa dhehebu? Kwa ishara ya kimbinguni, kwa mtu wa kimbinguni, aliyekuwa na huduma ya kimbinguni. Kumbukeni, Yeye habadiliki. Utukufu! Kama hilo lilitukia katika uzao wa kawaida, vipi kuhusu Uzao wa kimbinguni? Naam.

76 Mambo mengi, kama tungalikuwa na wakati wa kuyaingilia, yale aliyofanya katika uzao wa kawaida, jinsi alivyofanya hivyo kupitia uzao wa Isaka, yule, Isaka akiwa ndiye ule uzao, Baba

Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Jinsi ambavyo Eliya, manabii wengine wengi mashuhuri, wa kawaida . . . zile ishara kuu za kimbinguni walizofanya, lakini hao mashujaa wote wakuu walikufa. Lipo jambo moja walilopaswa kufanya ambalo ni kufa, kwa sababu walikuwa ni uzao wa kawaida.

77 Loo, Mungu abarikiwe! Lakini siku moja, kukaja Uzao wa kimbinguni, ambayo ilizaliwa kwa kuzaliwa kwa njia ya kimbinguni, imani ile ile, usiozaliwa kwa kuzaliwa kwa kawaida, bali kwa kuzaliwa kimbinguni, kwa imani ya kimbinguni aliyokuwa nayo Ibrahimu, si kulingana na tamaa ya kujuana kimwili ya Ibrahimu, na yale Mungu aliyomfanyia hivyo, bali kwa imani ya kimbinguni aliyokuwa nayo. Nayo imani ni ya kimbinguni, inafanya mambo ya kimbinguni.

78 Na kupitia kwa imani ya Ibrahimu, kama alivyokuwa hapa, mamia ya miaka baadaye, ukaja Uzao wa kimbinguni ambao aliuamini. Na wakati Uzao huu wa kimbinguni ulipokuja duniani, Yeye alifanya ishara ya kimbinguni ya Nabii wa kimbinguni. Alikuwa mkuu kuliko nabii, Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii kuwapa watu wa kawaida kuzaliwa kwa njia ya kimbinguni. Yeye alifanya nini? Alitutangulia, akafa, bali wasingeweza kumshikilia. Kaburi la Ibrahimu lingali pale, kaburi la Isaka lingali pale, bali kuna kaburi tupu juu ya Uzao wa kimbinguni uliofanya kazi ya kimbinguni, uliokuwa na ufufuo wa kimbinguni.

79 Yeye alifanya nini katika kufanya hilo? Alishinda mauti, kuzimu, na kaburi, na kumiliki malango yake, akafufuka siku ya tatu katika ufufuo wa kimbinguni, kasema, "Nina funguo za mauti na kuzimu." Amina. "Nilikuwa Yule aliyekuwa amekufa wakati mmoja, na sasa ni hai milele. Na kwa sababu Mimi ni hai, Uzao wa Ibrahimu utaishi, pia." Haya basi. "Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari. Na kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya."

80 Kumbukeni, Isaya alisema, "Itakuwa ni ishara ya milele." Alifufuka. Baadhi yenu ninyi watu msiojua habari zake, mnafikiri Yeye ni Mungu wa kihistoria, mkiabudu kitu kilichokuwa huko nyuma muda mrefu uliopita, bali Mungu yuyo huyo alifufuka katika wafu kama ishara ya kimbinguni, na baada ya miaka elfu mbili angali anaishi, angali papa hapa sasa, naye anaweza kutenda miujiza kama alivyofanya alipokuwa hapa duniani, kupitia kwa watu wa kimbinguni ambao wamezaliwa kwa Roho wa kimbinguni, pamoja na imani ya kimbinguni ambayo Ibrahimu alikuwa nayo katika jambo lile lile. Amina. Ishara, kweli, kwa ulimwengu katika siku za mwisho, kwamba Yeye angali hai.

81 Uzao wa Ibrahimu wa kimbinguni, watu wa kimbinguni, wasioitwa na madhehebu. Ningesema, "Je, wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mmethodisti."

“Wewe ni Mkristo?”

“Mi—mimi ni Mkatoliki.”

82 Hiyo inaonyesha wewe si Mkristo. Unaona? Kama wewe ni Mkristo, umezaliwa mara ya pili. Kama wewe ni Mmethodisti aliyezaliwa mara ya pili basi wewe ni Mkristo, si Mmethodisti, wewe ni Mkristo! Nalo neno *Mkristo* linamaanisha, “kuwa kama Kristo.” Na ikiwa wewe ni kama Kristo, Roho Wake anaishi ndani yako, nazo ishara hizi za ufufuo wa kimbinguni ziko pamoja nawe. Ishara za kimbinguni, nguvu za kimbinguni, ziko hai!

83 Uzao katika Isaka ulikuwa wa kawaida, huo ulikuwa uzao wa kwanza. Uzao wake wa pili ulikuwa ni imani, imani aliyokuwa nayo Ibrahimu katika Mungu iliyoleta uzao wa kawaida. Imani aliyokuwa nayo Ibrahimu katika Mungu iliubadilisha mwili wake alipokuwa mzee na kuleta uzao wa kawaida. Na imani iyo hiyo ikamleta Kristo duniani, kwa sababu ilikuwa ni ahadi ya Mungu, ambayo Mungu alikuwa amefanya kwamba angeituma ulimwenguni, nayo imani iyo hiyo katika ahadi iyo hiyo ndiyo ishara ya milele inayomleta Yeye miongoni mwa watu Wake, na kumfanya afufuke katika wafu, yeye yule jana, leo na hata milele. Amina.

84 Mbegu ya kawaida ni madhehebu, bila shaka; ule Uzao wa kimbinguni ni ishara. Naam. Unaweza kuiundia dhehebu. Hiyo ni kweli. Unaweza kuindia dhehebu. . .Huwezi kumwundia Mungu dhehebu, unaweza kuwaundia dhehebu kundi la watu. Huwezi kumwundia Mungu dhehebu, kwa sababu Yeye ni Ishara. Ninawaomba mlikasirikie. “Nitawapa ishara ya kimbinguni, ishara ya milele.”

85 Atakapokuja duniani, kile alicho wakati huo, atakuwa hivyo milele. Whiu! Yeye ni. . .Nilisahau tu jambo hilo, hata sikujua nilikuwa nikitokwa na jasho. Ni matone haya tu ya umande, ninatoa udenda sana, lakini nawaambia, mimi niko karibu sana na Kanaani, ninakula zabibu mpya, kwa hiyo itawafanya mtoe udenda. Amina.

86 Mungu wa kimbinguni alimfufua Yesu kimbinguni, na amemleta duniani akiwa hai, kwamba, katika Uzao wa Ibrahimu katika siku za mwisho, angeonyesha ishara ile ile ambayo Uzao wa kimbinguni ulisema, Uzao mkuu wa Ibrahimu, leo, utaamini kama Baba Ibrahimu alivyoamini, maana yule Mzao mkuu alisema hivyo, alipokuwa amesimama pale, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Yule Malaika, Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwao, alisimama huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, na kumwambia Sara yale aliyokuwa akiwazia, akamwambia Ibrahimu yale Sara aliyokuwa akiwazia na kufanya hemani.

87 Yesu alisema itakuwa ni ishara ya namna hiyo katika siku za mwisho, kwa sababu Yeye aliwaonyesha Wayahudi ishara ya kimbinguni ya Masihi, na kwa Wasamaria, baada ya kuwa na maelfu ya miaka ya mafundisho, lakini Mataifa hawakuyapata.

88 Sasa, ni ishara ya namna gani? Ishara ya kitheolojia? La, bwana. Ishara ya kimbinguni. Ni kitu gani? Masihi katika mwili wa kibinadamu. Utukufu! Ishara kuu, Roho Mtakatifu! Amina! Roho Mtakatifu, Masihi aliyefufuka akiishi ndani ya watu, Mzao wa Ibrahimu, anayeamini ya kwamba Yeye yuko. Nao Uzao ule ule wa kimbinguni utaamini kama baba yao, Ibrahimu, alivyoamini. Kama wao ni Uzao ule ule, wataamini ishara ile ile. Utukufu!

89 Madhehebu hayataamini hiyo, wataiita telepathia ya kiakili, wataiita ibilisi. Lakini Uzao wa kimbinguni wa Ibrahimu uliozaliwa kwa nguvu za kimbinguni za Mungu, unaamini ishara ile ile ya kimbinguni, kwa sababu Neno lile lile la kimbinguni lilisema hivyo. Amina. Ishara ya milele. Loo, jinsi ilivyo na nguvu, jinsi ilivyo kuu, jinsi Mungu wetu alivyo mtukufu! Ya kimbinguni, hakuna cha kawaida kuihusu, hakuna madhehebu yaliyoambatanishwa nayo, hakuna kanuni za imani za kujibunia, ni Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwa watu Wake pamoja na kuamini kwa kimbinguni. Amina. Mnaamini? Na tuinamishe vichwa vyetu basi.

90 Ee Mungu, Kiumbe cha kimbinguni, wakati unanipita. Wakati unatupita sote, Bwana, tunatambua mwaka mmoja tu uliopita, yale yaliyotukia katika mwaka uliopita, yanaendelea, yanapita haraka. Tunaona dunia ikifa, tunaona watu wakifa, tunaona majengo yakiporomoka, mataifa yakianguka, madhehebu yakishindwa.

91 Loo, tuna furaha sana kujua ya kwamba miongoni mwetu kuna Mtu wa kimbinguni, anayejitambulisha Mwenyewe kwa watu wanaoamini mambo ya kimbinguni. Mungu alisema angetupa Ishara kuu, nayo ingekuwa ni ishara ya Milele. Basi Bwana Mungu, unajithibitisha Mwenyewe kuwa Mungu wa Milele; Umefanya hivyo, utafanya hivyo, na sisi hapa katika siku za mwisho, wala haijawahi kuwa hivyo tangu Yesu alipokuwa hapa.

92 Kizazi hicho kilipokea ishara, ile ishara ya kimbinguni, nacho kikakosa kuiamini na kuingia katika machafuko. Nayo hii hapa baada ya wanatheolojia wote kujenga minara yao mikubwa ya Babeli, tunaona ya kwamba hawaoni ishara yoyote ya kimbinguni. Na sasa, katika saa hii ya mwisho umeshuka ukiwa na ishara ya kimbinguni miongoni mwa watu Wako kuita Uzao wa kimbinguni wa Ibrahimu, na kuwachukua watu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lako, ulisema ungefanya hivyo, na Wewe huyu hapa.

93 Maandiko yetu yanatwambia ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule, ishara ile ile. Jana Yesu alisema, "Ishara zile zile nizifanyazo, ninyi nanyi mtazifanya." Ninaomba Mungu, ya kwamba—ya kwamba wataliona na kuamini, na kumwamini Yesu Kristo kama Mwokozi wao.

[Dada mmoja ananena kwa lugha na ndugu fulani anafasiri—Mh.] Amina. Amina. Naam, Bwana.

Amina. Mungu ashukuriwe.

94 Je, kuna wengine hapa sasa ambao hawamjui Mungu, baada ya ujumbe huo, wangesimama kwa miguu yao na kusema, "Ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu binafsi"? Ni juu yako sasa, wewe ndiwe unayepaswa kufanya uamuzi, sasa hivi, amua upesi.

95 Asante, Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mtu mwingine? Mungu awabariki ninyi watatu. Mtu mwingine? Simama kwa miguu yako na kusema, "Nitamkubali kama Mwokozi wangu. Ninaamini kwa moyo wangu wote Neno la Mungu limefanyika mwili miongoni mwa watu siku hizi." Mungu akubariki, bwana.

96 Mtu mwingine? Inua mkono wako ama. . .useme, "Nikumbuke, nitaninii. . ." Mungu akubariki, mama. Mtu mwingine? Simama tu. Hatuna nafasi kwa ajili ya wito wa madhabahuni kuwaleta watu huku, tunawatakeni tu msimame na kushuhudia, namna hii, mkisimama, unaposimama, sema, "Ninamwamini Yesu Kristo Mwana wa Mungu, ninamkubali kama Mwokozi wangu."

97 "Mkinishuhudia mbele za watu, nitawashuhudia mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu." Je, kunaweza kuwa na wengine zaidi kabla ya kufunga, kabla hatujabadilisha ibada? Vema. Mungu awabariki. Mungu awabariki. Naam, wale wanaoinua mkono wao. Mungu akubariki, bwana. Mungu awe pamoja nawe, ndugu yangu. Mungu akubariki, bwana, unayesimama hapo umevaa shati jekundu. Mungu awe pamoja nawe; naam, na wewe, pia. Popote ulipo, Mungu akubariki, ndilo ombi langu.

Loo, "Amini tu, mambo yote yanawezekana, amini tu." Vema.

[Ndugu mmoja ananena kwa lugha na ndugu mwingine anafasiri—Mh.]

98 Hmm, hmm, hmm! Mnawezaje kulikataa enyi watu? Mngewezaje kufanya hivyo? Itakuwaje kama uko hapa bila Mungu, na-. . .na unajua ya kwamba umekosea? Kwa nini usisimame kwa miguu yako? Uisikie roho ikipiga makelele namna hiyo kote kwenye Neno la Mungu namna hiyo!

99 Baadhi yenu Wakristo mliosimama karibu na mtu huyo aliyesimama hapo, hivi mwaweza tu kuzungumza naye, na kuomba pamoja naye hapo? Mahali hapa pamejaa kabisa hapa hatuwezi kufanya wito wa madhabahuni. Na wale waliosimama,

Mkristo fulani aliye karibu nao anayewajua, zungumzeni tu nao sasa kuhusu nafsi yao, waambieni ya kwamba Yesu anawasamehe.

100 Mungu anakusamehe, ndugu yangu, wewe uliyesimama hapo kwa miguu yako. Bila shaka. Kama ukisimama . . . Unamwamini Yeye kama Mwokozi wako? Unamtaka Yeye . . .? Unaamini ya kwamba Yeye anakuokoa? Basi umeokoka, ndugu yangu. Vic, wewe ni mmoja wetu sasa, endelea moja kwa moja katika Ufalme wa Mungu, naam, bwana, kama unaweza kuamini kwa moyo wako wote.

101 Je, kuna wengine ambao wangesimama na kusema, kwa kusimama tu, wakisema, "Ninamkubali, ninamwamini, ninaamini Ujumbe ni wa kweli"? Mungu awabariki huko nyuma, Bwana awasamehe ninyi nyote—ninyi nyote hapo. Kila mmoja, ninyi mlio hapo, Wakristo, waambieni kile Mungu anachomaanisha kwao.

102 Chini kupitia kwenye marefu haya ya kanisa, kuna yeyote chini kupitia hapa angesimama? Aseme, "Nitamkubali mimi mwenyewe, papa hapa." Yeyote huko chini kwenye marefu haya ya kanisa? Mungu awabariki, huko nyuma na kote juu chini upande huu. Mungu akubariki, bwana.

103 Ninyi Wakristo mlio karibu nao, nyosheni mkono, na kuushika mkono wao na kusema, "Mungu akubariki." Huko kwenye marefu ya kushoto, kule, huko mbali sana kwenye . . . mtu yeyote humo awezaye kusimama na kusema, "Nitamkubali sasa kama Mwokozi wangu"? Unawezaje kulikataa, ndugu, wakati hili hapa Neno, na Roho, na nguvu, na ishara? Ulimwengu unataka mwujiza fulani, unataka kitu fulani kikuu, hiki *hapa*, nguvu za kimbinguni, nguvu kuu.

104 Vema. Nilikuwa nikienda, niwaombe ndugu zangu wahudumu waambatane nami leo kuwaombea wagonjwa, kusudi watu wafahamu dhahiri ya kwamba Kristo huwaponya wagonjwa, na ya kwamba mambo yote kwa . . .

[Dada mmoja ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu fulani anafasiri—Mh.] Hmm! Mungu asifiwe. Amina. [Ndugu fulani ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mwingine anafasiri. Dada fulani anatabiri.]

Amina. Tunamshukuru Bwana. Amina.

105 Sasa mnasikia yale Roho anayowaambia watu. Mnaona? Hiyo inamaanisha kwamba, Chicago, huenda mnapokea kitu fulani, mnaona. Na huenda ikawa ndiyo mara yenu ya mwisho, kwa hiyo kama kuna shaka lolote, Roho amenena hapo hata mara nne, mnaona, vema sasa, m—mnapaswa kujitolea kwa Kristo. Kuna mtu hapa ambaye hajafanya hivyo? Simama, ama, inua tu mkono wako, useme, "Unikumbuke, Ee Bwana, nikumbuke."

106 Mungu awabariki. Hebu. . .Mungu akubariki, ewe kijana. Mungu akubariki. Vema. Mungu akubariki, ewe kijana. Kuna vijana wawili. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, mama. Mungu ambariki maskini mama huyo, pia. Naam, hilo ni sawa. Anakuona na anakujua, anajua yote kukuhusu. Mungu yeye yule aliyemfufua Yesu katika wafu yupo hapa sasa. Mnaamini?

[Ndugu fulani ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mwingine anafasiri. Dada fulani anatabiri. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Amini tu, amini tu,
Yote. . .

Hizo ni ishara. Angalieni yale anayofanya sasa, angalieni yale anayofanya.

Amini tu, amini tu,
Yote. . .

107 Ni wangapi walio wagonjwa? Inua mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa, Ndugu Branham, ninahitaji usaidizi kutoka kwa Mungu, mimi ni mhitaji." Mungu awabariki. Iweni tu na kicho kabisa, ketini kimya kabisa, kwa muda kidogo tu. Jalia Roho Mtakatifu. . . Sasa, tumeona ishara, ishara za uwepo Wake, sasa angalieni mwone kama Yeye hataonyesha Ishara Kuu.

108 Nilikuwa nikitaka kuwaita wahudumu hapa chini kuwaombea wagonjwa, lakini Roho Mtakatifu, nilipomsikia akinena kupitia kwa watu, *kitu fulani* kilishuka tu, sina karama ya kunena kwa lugha wala kufasiri, ni karama nyingine, nami nikawazia, "Bwana, ni nini kulingana na watu hao?" Akasema, "Hiyo ndiyo ishara."

109 Sasa hii hapa ishara kuu inakuja. Uh-huh. "Nitawapa, katika siku hizi za mwisho, ishara kuu, ishara kuu."

110 Ombeni, mwaminini Mungu, ninyi nyote, aminini tu ya kwamba Mungu atawaponya, tuone kama Yeye angali ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Rahisi sana sasa. Inueni vichwa vyenu na mwangalie *huku*, niaminini mimi kuwa ni mtumishi Wake, mtaona kama ni kweli ama si kweli.

111 Ombeni. Jiombee tu mwenyewe. Mtu fulani aseme, "Bwana Yesu, jalia niguse vazi Lako. Wananiambia Wewe ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Mwanamke mmoja wakati mmoja aligusa vazi Lako, ukageuka na kumwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, kisha ukasema imani yake ilikuwa imemwokoa. Jalia nikuguse Wewe, Bwana, nione kama ni kweli." Amini tu.

112 Huyu hapa maskini mwanamke mmoja ameketi papa hapa, amevaa nguo ya kijani kibichi, mwanamke mweusi. Naam. Unaombea jambo fulani. Mwanamke mdogo, mwembamba. Je,

una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi. Nilitaka tu kujua kama ungekuwa mstarini au la, unaona. Huna kadi ya maombi.

113 Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, utaniamini? Hujiombei mwenyewe, unamwombea mama yako. Hayupo hapa, yuko katika jimbo la Tennessee. Hiyo ni kweli. Unataka nikwambie anaugua nini? Je, utaamini kwa moyo wako wote basi? Ana uvimbe tumboni mwake. Hiyo ni BWANA MUNGU ASEMA HIVI.

114 Sijawahi kumwona huyu mwanamke maishani mwangu. Hiyo ni kweli, mama? Hatufahamiani kabisa? Mwanamke tu, ndio kwanza tu aingie na kuketi chini pale. Hiyo ni kweli. Yote ni kweli? "Tazama, nitawapa ishara ya milele." Yesu amefufuka katika wafu. Aligusa *Kitu fulani*.

115 Huyo hapo mwanamke ameketi, ameketi papo hapo nyuma. Anaugua ninii, ana u—ugonjwa wa mgongo, na ugonjwa wa figo. Huyo mama mweusi, aliyeketi moja kwa moja huko nyuma katika mkono wa kushoto, nyuma hapa, ananiangalia. Anatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Bibi Frane, pokea uponyaji wako pamoja na Roho Mtakatifu.

116 Angalieni kama hiyo ni kweli. Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu. Kama hiyo ni kweli, mama, punga mkono wako huku na huku. Lakini kama hayo ndiyo mambo unayotafuta, na kwamba yanahusu nini, kama yote yalikuwa ni kweli punga tu mkono, endelea tu kupunga mikono yako. Vema. Nenda, nawe unaweza kupata kile unachoomba, maana uligusa ishara kuu. Amina.

117 Unaamini kwa moyo wako wote? Kuna mwanamke mwingine aliyeketi nyuma yake, moja kwa moja kule nyuma. Na mwanamke huyu, yeye anatafuta jambo kuu pia, bali ni mtoto mchanga. Bibi Cary, kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kumpokea mtoto wako, ninakutumia katika Jina la Yesu Kristo.

118 Simjui mwanamke huyo, hatufahamiani kabisa. Lakini kama hiyo ni kweli, mama, simama, kama kila kitu ni kweli, na kila kitu kilichosemwa ni kweli. Vema. Mungu akubariki. Kama hatufahamiani, punga mikono yako *hivi*. Vema. Vema. Utapokea ishara kuu. Amina.

Mnaona, Yeye angali ni Mungu. Amina. Unaamini kwa moyo wako wote? Iweni tu na imani.

119 Huyu hapa msichana mweusi ameketi, ameketi papa hapa mwishoni mwa safu, anaugua ugonjwa wa moyo. Sikujui, mama. Wewe hutoki hapa, unatoka Zion, Illinois. Jina lako ni Bibi Fitzgerald. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako, dai imani yako katika Mungu aliye hai. Mungu akubariki. Nenda, amini.

120 Mama huyo mweusi aliyemsaidia kule juu, pia anaugua, una TB ya uti wa mgongo. Na jina lako ni Binti Davis, nawe unatoka Zion. Huyo mama aliyemsaidia ni dada ya msichana huyu mwingine. Jina lako ni Fitzgerald, pia, nawe unatoka Zion. Hiyo ni kweli. Ni kweli. Nawe una ugonjwa wa koo, lakini umeponywa, Yesu Kristo akuponya. Amina.

Unaamini kwa moyo wako wote? Vipi kuhusu mtu fulani huko nje namna hii?

121 Bibi Smith, mwenye shinikizo la chini la damu, unaamini Yesu Kristo anakuponya? Kama unaamini, Bibi Smith, simama kwa miguu yako, likubali, na uliamini kwa moyo wako wote. Utaponywa, shinikizo la chini la damu linakuacha.

Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini hiyo ni kweli. Unaamini? Mwamini Mungu, usiwe na shaka.

122 Mtu fulani alinigusa ubavuni mwangu, ambaye nadhani alikuwa ni mwanangu anayewazia ya kwamba karibu nimefanya ya kutosha. Amini tu kwa moyo wako wote.

Binti Bailey, usitie na shaka, bali mwamini Bwana Yesu Kristo nawe utaponywa. Rudi huko Gary na uwaambie jinsi Mungu alivyo mkuu.

123 Unaamini? "Tazama, nitawapa ishara kuu." Mungu aliyedhihirishwa katika mwili! Hivi hamwezi kuiona, Chicago, baada ya miaka hii yote ambayo nimekuwa hapa pamoja nanyi? Mungu akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu, kwa neema ya Yesu Kristo. "Ninawapa ishara kuu."

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

124 Kila mtu aliye na kadi za maombi, inua mkono wako. Shikilia kadi yako ya maombi mkononi mwako. Mnaniamini mimi kuwa mwonaji Wake, nanii Wake...? Mnaamini ya kwamba si mimi, mimi—mimi—mimi ni ndugu yenu? Mnaamini? Mnaamini ya kwamba Mungu amelithibitisha Neno Lake, kwamba tuna ishara ya kunena kwa lugha na kufasiri, halafu ishara kuu ya kufufuka Kwake?

125 Kama mnaamini, nitaninii, katika Jina la Yesu Kristo, nitawatangaza kila mmoja wenu kuwa ni mzima, kama mnaamini, nawe utaangusha kadi yako. Angusheni kadi zenu sakafuni, iangushe tu kadi yako. Jambo ndilo hilo. Pokeeni uponyaji wenu! Tupeni tu kadi zenu sakafuni, na

kusema, "Ninamwamini Mungu. Hilo linatosha kwangu! Sasa hivi, ninamwamini Mungu." Rusheni kadi zenu juu, mseme, "Ninathibitisha ninaamini kwa moyo wangu wote ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anaishi na kutawala na . . ." Utukufu!

61-0430 Ishara Kuu
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org